









Wound Care after stitches (Swahili)

Kutunza jeraha baada ya gundi au kushonwa



Jeraha la mtoto wako limerekebishwa na nyuzi za kushonea au gundi ili kupunguza damu, kukuza uponyaji na kupunguza makovu.

Utunzaji wa nyumbani

Gundi	Ushonaji
<p>FANYA</p> <ul style="list-style-type: none">  Acha mkanda/steri-strips zianguke kawaida. Zikijikunja, zikate tena.  Weka jeraha kavu kwa siku 5. Mtoto wako anaweza kuoga kwa muda mfupi baada ya masaa 24. Kausha jeraha kwa kitambaa. 	<p>FANYA</p> <ul style="list-style-type: none">  Weka jeraha kavu kabisa kwa masaa 24 ya kwanza. Baada ya hayo, epuka kuloweka jeraha na ukauke kwa upole na kitambaa baada ya kuoga.
<p>USIFANYE</p> <ul style="list-style-type: none">  Usitumie krimu au marashi mpaka gundi imetoka.  Usimruhusu mtoto wako kusugua, kukwaruza au kuondoa gundi au sehemu za steri.  Usimruhusu mtoto wako kuogolea. 	<p>USIFANYE</p> <ul style="list-style-type: none">  Usimwache mtoto wako aondoe vigaga vyovyote karibu kwenye jeraha.  Usimruhusu mtoto wako kuogolea hadi mishono huondolewa.
<p>Gundi itatoka yenyewe kama jeraha linapoona. Hii kwa kawaida inachukua kati za siku 5 na 10.</p>	<p>Ikiwa mtoto wako ana mishono isiyoweza kuyeyushwa, daktari wako atahitaji kuiondoa.</p> <p>Ikiwa mtoto wako ana mishono inayoweza kuyeyushwa, itatoka yenyewe baada ya muda.</p>

Jeraha huponyaje?

Jeraha la mtoto wako litakuwa jekundu na laini wakati linapoona. Mtoto wako anaweza kuhitaji dawa rahisi za maumivu kama vile paracetamol (Panadol au Dymadon) na ibuprofen (Nurofen). Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kipimo cha sahihi. Usimpe mtoto wako kipimo zaidi ya kile kinachopendekezwa kwa siku. Inapaswa kujisikia vizuri zaidi baada ya siku 2 au 3.

Majeraha yote yataweka kovu. Kovu linaweza kuwa jekundu au la zambarau kwa rangi na litafifia hadi kuwa waridi isiyokolea au nyeupe au kuwa karibu kutoonekana (linaweza kuchukua hadi miezi 12).



Unawezaje kuboresha mwonekano wa kovu la mtoto wako?

- Weka jeraha lisiwe kwenye jua unapoweza na tumia mafuta ya kuzuia jua.
- Kanda jeraha kwa shinikizo kali mara kadhaa kwa siku na krimu ya kuchepesha kama vile Sorbolene.

Zungumza na daktari wa watoto wako ikiwa una wasiwasi kuhusu jinsi kovu linavyoonekana. Mwelekezo wa kumuona daktari wa upasuaji wa plastiki unaweza kuhitajika ikiwa jeraha halipone kama inavyotarajiwa.

Wakati wa kuonana na daktari

Mwona GP wako ikiwa:

- jeraha hufungua tena au hutoka damu katika masaa 48 ya kwanza
- jeraha huvimba na/au nyekundu karibu na kingo
- uwekundu karibu na jeraha huenea kwa ngozi inayozunguka
- mtoto wako anapata homa
- jeraha lina harufu au kuna umajimaji wa njano au kijani.

Ikiwa huwezi kumwona daktari wako, tafadhali kwenda kwa idara ya dharura iliyo karibu nawe.

Kwa ushauri wa matibabu usio wa dharura, piga simu **13 HEALTH** (13 43 25 84) kuzungumza na muuguzi aliyesajiliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa gharama ya simu ya mtaa.



Omba kupata mkalimani ikiwa unamhitaji.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi.

Resource ID: FS086 **Reviewed:** July 2022

Kanusho: Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.